

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5  
*Fax No.* +255 026 2322624  
**E-mail:** [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUANZA KWA  
VIKAO VYA KAMATI ZA BUNGE TAREHE 15 HADI 27  
JANUARI, 2018, MJINI DODOMA**

---

**1.0 UTANGULIZI**

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana Jumatatu tarehe 15 hadi tarehe 27 Januari, 2018 Mjini Dodoma kutekeleza majukumu ya kibunge kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Kumi wa Bunge uliopangwa kuanza tarehe 30 Januari 2018. Kwa mujibu wa ratiba ya shughuli za Kamati, Waheshimiwa Wabunge wote wanapaswa kuwasili Mjini Dodoma Jumapili tarehe 14 Januari, 2018 tayari kwa kuanza vikao vya Kamati.

Katika kipindi cha vikao hivyo, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Kamati ni kama **ifuatavyo**:

**a) ZIARA ZA UFUAMILIAJI**

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati Tatu (3) zitafanya ziara za ufuamiliaji katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati hizo ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa - LAAC, Kamati ya Hesabu za Serikali - PAC pamoja na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utaliiii.

**b) UCHAMBUZI WA MISWADA MBALIMBALI NA KUPOKEA MAONI YA WADAU**

Kamati Tatu (3) za Kisekta zitakuwa na shughuli za uchambuzi wa Miswada ya Sheria kama ifuatavyo;

- i) Kamati ya **Katiba na Sheria** itachambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2017 [**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017**]. Kamati hiyo pia itakuwa na kikao cha kupokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada huo siku ya Jumanne tarehe **16 Januari, 2018** kwenye ukumbi uliopo katika **Ofisi ya Bunge** Mjini Dodoma kuanzia **saa tatu kamili (3:00) asubuhi hadi saa Tisa (9:00) Alasiri.**
- ii) Kamati ya **Ardhi, Maliasili na Utalii** itachambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Mwaka 2017 [**The Wildlife Conservation (Amendment) Bill, 2017**]. Kamati hiyo pia itakutana na kupokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada huo siku ya Jumanne tarehe **16 Januari, 2018** kwenye ukumbi uliopo katika **Ofisi ya Bunge** Mjini Dodoma kuanzia **saa tatu kamili (3:00) asubuhi hadi saa Tisa (9:00) Alasiri.**
- iii) Kamati nyingine ni Kamati ya **Huduma na Maendeleo ya Jamii** ambayo itachambua Muswada wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2017 (**The Public Service Security Fund, Bill, 2017**) na itakuwa na siku mbili (2) za vikao vya kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada huo siku ya **tarehe 17 na 18 Januari, 2018** kwenye ukumbi uliopo katika **Ofisi ya Bunge** Mjini Dodoma kuanzia **saa tatu kamili (3:00) asubuhi hadi saa Tisa (9:00) Alasiri.**

***Wadau wote katika Miswada iliyotajwa hapo juu wanakaribishwa kufika mbele ya Kamati kutoa maoni yao katika tarehe na muda uliotajwa.***

**c) KUPOKEA TAARIFA ZA KIUTENDAJI WA WIZARA**

Kamati Tisa (9) za kisekta zitaendelea kupokea Taarifa za kiutendaji wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (c) na (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo Januari, 2016.

Aidha, Kamati ya Bajeti pamoja na shughuli nyingine itapokea maoni ya wadau wa Utalii kuhusu Mwenendo wa shughuli za Utalii baada ya kuanzisha utozaji wa VAT kwenye shughuli za Utalii.

**2.0 KUMBI ZITATAZOTUMIKA**

Tofauti na hapo awali kwa sasa Kamati zote zitakutana kwenye kumbi zilizopo katika Ofisi ya Bunge mjini Dodoma. Uamuzi huu umefikiwa baada ya kubaini yafuatayo;

- Ukubwa wa gharama kwa kukodi kumbi nje ya Ofisi ya Bunge,
- Usumbufo kwa Wabunge kutokana na umbali wa kumbi zilipo,
- Ugumu wa uratibu kutokana na kutawanyika kwa kumbi,
- Usumbufo kwa wadau wanaoalikwa kwenye kamati na;
- Changamoto ya Utoaji wa huduma muhimu zinazofanikisha shughuli za Kamati.

Hivyo, changamoto zote hizo zinatatuliwa kwa Vikao vya Kamati zote kufanyika katika eneo moja la Ofisi ya Bunge ambapo huduma zote muhimu kiutawala, utaratibu, afya, ulinzi na ustawi wa Wajumbe zitapatikana kwa urahisi, ubora, uharaka na zaidi **kupunguza ghamara na kuongeza ufanisi.**

Ratiba zote za Shughuli za Kamati za Bunge ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo kamati hizo zitafanya ziara, pamoja na Miswada itakayo shughulikiwa na Kamati katika kipindi hiki vinapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz).

**Imetolewa na:** Kitengo cha Habari, Elimu kwa Umma na Mawasiliano  
Ofisi ya Bunge  
**DODOMA**

**12 Januari, 2018.**